# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL 4
# KISWAHILI PAPER 1 ANSWERS

**1. (i) Hii ni barua rasmi.**

**-Ina anwani mbili na tarehe.**

**(ii)Kuna mtajo:kwa Bw/Bi,**

**(iii) Kusudi:MINT/KUMB/KUH:MAOMBI YA KAZI.**

**(iv) Uraia wako.**

**(v) Jinsia/uana wako.**

**(vi)Umri wako.**

**(vii) Masomo.**

**(a) Shule ya msingi (wapi?ukapata alama ngapi?)**

**(b) Shule ya sekondari (wapi?ukapata nini?)**

**(viii)Wadhifa katika shule ya msingi.**

**(ix)Wadhifa katika shule ya sekondari**

**(x) Mafunzo ya kazi (wapi?lini?ukapata cheti kipi?)**

**(xi) Wadhifa katika chuo cha mafunzo. (xii)Kazi –ulifanya wapi?lini.**

**(xiii)Ujuzi-miaka mingapi? (xiv) Uraibu-unapenda nini?**

**(xv) Tamati.**

**-Ndimi wako mwaminifu,**

**- Sahihi.**

**- Jina mahsusi.**

**- Cheo chako.(si lazima)**

**(xvi) Warejelewa.**

**- Wawe wawili na anwani au simu zao. * Mtahiniwa akipotoka kimtindo :apoteze alama 4.**

**2. Hii ni insha ya mjadala. Faida ya serikali ya ugatuzi.**

**(i) Ajira nyingi zimezalishwa.**

**(ii) Rasimali kutumiwa na wananchi wenyewe.**

**(iii)Miundo msingi kuboreshwa.**

**(iv) Maendeleo kusawazishwa kote nchini.**

**v) Utawala kuwa karibu na wananchi.**

**(vi) Kuleta huduma muhimu karibu na watu.**

**(vii) Kushirikisha jinsia zote uongozini.**

**(viii) Usalama umeimarishwa. Hasara za serikali ya ugatuzi**

**(i) Kuongezeka kwa kodi.**

**(ii) Gharama ya maisha imepanda-watawala ni wengi.**

**(iii)Tofauti za kimaendeleo.**

**(iv) Zimekuza hisia za kikabila.**

**(v) Mkanganyo kati ya serikali kuu na majimbo.**

**(vi) Majimbo yasiyo na rasimali ya kutosha yamebaki nyuma.**

**(vii) Mapendeleo katika kutoa ajira.**

**(viii) Kujiuzulu kwa watalaamu, n.k TANBIHI**

***Hoja za kila upande zisipungue tano.**

***Mtahini ahakikishe hoja zingine za mtahiniwa.**

**3. Udongo Uwahi ungali maji.**

**i) Hii ni insha ya methali.**

**(ii) Mtahiniwa atunge kisa kinachooana na methali**

**(iii)Mtahini akamilishe kisa kwa kutoa funzo.**

**Anaweza kumaliza na methali iyo hiyo.**

**4. Insha ya mdokezo.**

**(i) Mtahiniwa amalize insha kwa maneno aliyopewa.**

**(ii) Aonyeshe sababu ya kutamani kuona babake.**

**(iii)Ajihusishe moja kwa moja.**

**(iv) Aonyeshe sababu iliyopelekea asimwone babake tena.**

***Mtahiniwa akipotoka apate alama 20 02**

**NAMNA YA KUTUZA**

**1. Maki 01- 05**

**Insha haileweki kwa vyovyote.**

**Lugha ni hafifu sana.**

**Lugha isiyo sahihi-ukosefu wa ubunifu,makosa ya kisarufi na hijai,mtindo mbaya,n.k 2.**

**2 Maki 06 -10**

**Mawazo yamewasilishwa lakini kwa njia isiyoeleweka kikamilifu**

**Kujirudiarudia.**

**Makosa ya kisarufi/hijai.**

**3. Maki 11-15**

**Mtahiniwa amedhihirisha kuimudu lugha.**

**Ametumia miundo sahihi ya sentensi.**

**Ubunifu umedhihirika.**

**Insha inaeleweka na ina mtiririko.**

**4. Maki 16 -20**

**Insha ina mtiririko.**

**Maudhui sahihi yamekuzwa.**

**Kuna ubunifu.**

**Ametumia tamathali za usemi.**

**Mawazo yamewasilishwa kwa mpangilio unaovutia.**

**Makosa yote yasizidi matano.**

**MAMBO YA KUANGALIA.**

**(i) Urefu.**

**(ii) Hati.**

**(iii)Uakifishaji.**

**(iv) Mtindo ya kuandika baadhi ya herufi ambayo si sahihi.**

**(v) Unadhifu wa kazi.**

**(vi) Sura ya insha.**

**MAKOSA YA HIJAI**

**(h)**

**(i) Kutenganisha neno k.m aliye kuwa.**

**(ii) Kuunganisha maneno k.m kwasababu.**

**(iii)Mwendelezo mbaya wa neno.**

**(iv) Kuandika maneno kifupi.**

**(v) Kukatia neno kwenye konsonanti//kulikata mwishoni bila kuweka kistari n.k.**

**MAKOSA YA SARUFI**

**(s)**

**(i) Kuakifisha vibaya.**

**(ii) Kutumia herufi kubwa ama ndogo mahali si pake.**

**(iii)Matumizi mabaya ya ngeli,nyakati na mnyambuliko.**

**(iv) Kuacha au kuongeza neno katika sentensi k.m kwa kwa n.k.**